Swahili Colloquium
Bayreuth

UNIVERSITÄT
BAYREUTH

# KONGAMANO LA ISHIRINI NA SABA LA KISWAHILI
# Bayreuth, tarehe 8 hadi tarehe 11 mwezi wa sita 2014

Tarehe 14, mwezi wa
Januari, 2014

Wapendwa mabibi na mabwana!

Tuna furaha kubwa kuwaalika kwenye kongamano la ishirini na saba litakayofanyika hapa Ujerumani katika Chuo Kikuu cha Bayreuth.

**Kongamano la Kiswahili**

Kongamano letu la Kiswahili limeshaota mizizi hapa Chuo Kikuu cha Bayreuth. Kila mwaka linawakaribisha watalamu wa masomo mbalimbali wanaofanya uchunguzi kuhusu vipengele kadha wa kadha vya Kiswahili (ama Viswahili) na tamaduni zao. Upana wa mada zinazohusu Kiswahili na zinazozungumziwa kwenye Kongamano, kuanzia isimu, masomo ya fasihi mpaka anthropolojia na historia ni msingi wa nguvu ya kongamano hili. Watalamu kutoka pembe mbalimbali za dunia na masomo anuwai wanapata kubadilishana mawazo. Pia tunawakaribisha mashabiki na wasanii wa fani mbalimbali za Kiswahili. Zaidi ya kuwakaribisha wale ambao wamezoea kuja Bayreuth, pia tunafurahi kuwakaribisha watalamu na wanafunzi wapya kwetu.

**Mradi wa Kongamano la Kiswahili wa mwaka huu**

Mwaka huu mradi wa kongamano la Kiswahili ni tofauti kidogo na miradi ya miaka iliyopita.

Kwanza, Kongamano la Kiswahili halitaanza siku kuu ya Kupaa kwa Yesu Mbinguni (“Ascension Day”) kama ilivyokuwa desturi yetu. Mwaka huu, Kongamano limepangwa **lifanyike mwezi wa sita** ili likaribie makongamano mawili muhimu yatakayofanyika Bayreuth wiki hiyo pia: Chuo Kikuu cha Bayreuth kitakuwa na Kongamano la Wanaisimu wa Lugha za Kiafrika (“Afrikanistentag”) tarehe 10 na tarehe 11 mwezi wa sita. Aidha, Kongamano la Masomo ya Kiafrika Ujerumani (“VAD”) litafafnyika kuanzia tarehe 11 mpaka tarehe 14 mwezi huo huo.

Pili, mwaka huu tutakuwa na warsha maalum yenye anwani: **“Mienendo Mipya katika Masomo ya Kiswahili”** (“New Dynamics in Swahili Studies”) ambayo itakuwa ni sehemu ya Kongamano la Kiswahili. Warsha hiyo itaandaliwa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Leipzig na wahariri wa Swahli Forum ili kusherekea miaka 20 ya jarida “Swahili Forum”. Madhumuni ya warsha hiyo itakayokusanya wageni maalum walioalikwa kutoka nyanja mbalimbali ni kujadili historia na maendeleo ya masomo ya Kiswahili, hali yake sasa na changamoto zilizoko na maono ya miaka ijayo. Mnakaribishwa kusikiliza hotuba zitakazowasilishwa wakati huo pia.

**Mada maalum**

Kongamano la Kiswahili la mwaka huu litakuwa na mada maalum ifuatayo: **“Kiswahili na Vyombo Vipya vya Habari na Teknolojia”** (“Swahili and New Media and Technologies”). Kwa kufuata mada maalum ya “Afrikanistentag”, mada hii inapendekeza kuchunguza na kujadili maswali yanayohusu uhusiano baina ya vyombo vipya vya habari na technolojia mpya kwa upande mmoja na lugha ya Kiswahili kwa upande mwingine. Kwa ajili ya maendeleo mapya ya hivi karibuni, nyanja mpya zimeibuka zinazoipatia lugha za Kiafrika kama Kiswahili nafasi mpya na umuhimu zaidi. Tofauti na kuchapisha vitabu ama katika majarida ya kawaida ambako mara nyingi ni kwa wachache tu wanaojiweza, nafasi hizi zinawapatia watu wengi zaidi nafasi ya kuwasiliana, kutoa maoni, kufundisha, kuandika na kutoa fasihi kwa lugha ya Kiswahili. Ingawa mawasiliano-jamii (‘social media’), kama Facebook na Twitter, na tovuti kama Youtube, na pia blogu na vyumba vya chat pamoja na simu za mkono na ‘vitanzu vyake’ vya hivi karibuni vinatumika sana Afrika Mashariki, athari zao kwenye matumizi ya lugha na mazingira yake hazijachunguzwa kwa undani mpaka sasa.

“Kiswahili na Vyombo Vipya vya Habari na Teknolojia” itakuwa ni mada maalum katika kongamano la mwaka huu. Lakini, kupendekeza mada maalamu hakumaanishi kwamba hatutakubali mada nyingine. Ikiwa unapendelea kuzungumzia mada nyingine, pia usisite kujiandikisha.

**Kujiandikisha**

Tunaomba mada zenu katika lugha ya Kiswahili ama Kiingereza. Kila uwasilishaji wa mada pamoja na majadiliano unakadiriwa kuchukua muda wa dakika thelathini tu. Tafadhalini, mjiandikisheni kwa njia ya baruapepe (swahili@uni-bayreuth.de) mpaka kufikia tarehe **31 Machi 2014**. Iwapo mtatoa makala yenu kwa Kiswahili, tafadhalini muandike pia muhtasari mfupi kwa Kiingereza. Tafadhalini, mjiandikishe pia hata ikiwa hamtatoa makala na/ama mkitaka kuhudhuria katika warsha ya „New Dynamics“.

**Pahala/wakati**

Pahala pa Kongamao hapajathibitishwa. Mtapata habari zaidi katika barua itakayofuata. Kongamano limepangwa lianze siku ya Jumapili, tarehe 8, saa tatu asubuhi.

**Malazi**

Kwenye ukurasa wa mtandao mtapata habari za malazi. Iko orodha ya hoteli pia (maelezo hayo yanatokana na Idara ya Utalii ya mji wa Bayreuth). Tena wanafunzi wetu watawakaribisha wanafunzi kutoka vyuo vikuu vyingine wakae nyumbani mwao kwa muda wa kongamano. Wanafunzi wanaotaka kupata malazi kwa mtu binafsi, watuarifu mapema kwa njia ya baruapepe (tazama anwani yetu chini). Tena, wanafunzi (chini ya umri wa miaka 25) wanaweza kupata malazi katika “Bweni la Vijana” (tazama http://www.jugendherberge.de/jh/bayern/bayreuth/).

Muda si mrefu unaweza kupata barua hii, ratiba na habari mpya kwenye ukurasa wa mtandao ufuatao:

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html

Barua ya pili ya mwaliko itakayoambatanishwa na mpangilio wa makala na utaratibu mzima wa kongamano itatumwa mwisho wa mwezi wa nne (Aprili).

Ikiwa mna maswali, msisite kutuandikia. Kwa mawasiliano zaidi, tumieni anwani yetu ya email: swahili@uni-bayreuth.de ama clarissa.vierke@uni-bayreuth.de

Tukiwa na matumaini ya kuonana katika Kongamano hili la 27 la Kiswahili hapa Bayreuth twasema "Karibuni Sana."

Dr. Clarissa Vierke & Prof. Gabriele Sommer

Afrikanistik I
Universität Bayreuth,
95440 Bayreuth
Tel.: +49-921-553556
Fax.: +49-921-553641